SERA G011:SERA YA USIRI

Mhusika	Mkurugenzi Mkuu	Toleo:	2.1
Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi Tarehe:	27 Februari 2019	Tarehe ya Kufanyiwa Mapitio:	Februari 2025

DIBAJI

Sera hii iliandikwa na Shirika la So They Can (International) lililopo Australia kwa ajili ya kutumika katika ofisi zote za So They Can. Shirika la So They Can lina ofisi tano zilizosajiliwa katika nchi ya Australia, Kenya, Tanzania, New Zealand na Marekani ambazo ni sehemu ya So They Can Global Alliance. Katika sera hii "Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa So They Can (International).
Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo "Bodi" maana yake ni bodi ya So They Can (International).
Sera hii inawalenga wafanyakazi wote wa So They Can, Wajumbe wa Bodi na wafanyakazi wakujitolea katika ofisi zote 5 za So They Can. Taratibu za So They Can zinaendana na sera za So They Can.

UTANGULIZI

So They Can linawajibika kulinda taarifa zako binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya Usiri ya Australia iliyomo katika Sheria ya Usiri ya mwaka 1988.
Sera hii ina taarifa za namna So They Can inavyokusanya, tumia, kutoa na kuhifadhi taarifa binafsi ikijumuisha taarifa nyeti na namna mtu anavyoweza kupata na kurekebisha taarifa binafsi tulizonazo.

UFAFANUZI

Taarifa Binafsi maana yake ni taarifa au maoni kuhusu mtu aliyebainishwa au mtu anayebainishwa ikiwa:

- taarifa au maoni ni ya kweli au la; na
- taarifa au maoni yamehifadhiwa katika muundo wa nyaraka au la.

SERA

NI TAARIFA GANI TUNAKUSANYA

So They Can wanaweza kusanya taarifa binafsi kutoka kwa watu ambao wanahusika katika uendeshaji na katika shughuli zetu ikijumuisha wafanyakazi, wahisani, washiriki wa utafiti, wanufaika, washiriki katika kampeni za kukusanya fedha, wajumbe, wasambazaji, wafanyakazi wa kujitolea na watoahuduma.
Taarifa ambazo So They Can inakusanya na kuzihifadhi zinajumuisha:

- Jina lako, anwani, namba ya simu, baruapepe (taarifa za mawasiliano)
- Tarehe ya kuzaliwa, jinsia, kipato na kazi
- Taarifa za mwajiri wako, kama ni mfanyakazi kwa kuwasilisha
- Taarifa za kadi yako ya benki au ya mkopo
- Historia yako ya uchangiaji, baruapepe, barua na uhusiano mwingine na So They Can

TUNAKUSANYAJE TAARIFA BINAFSI

Pale inapowezekana So They Can itakusanya taarifa zako binafsi kutoka kwako moja kwa moja. Hii inaweza kufanyika kwa kuwasiliana na wewe moja kwa moja au kwa baruapepe, kwa simu au kwa mtandao. Tunaweza kukusanya taarifa binafsi kutoka kwa chanzo kingine ikijumuisha upande wa tatu ambao umeomba ridhaa,

pale ambapo hakuna sababu za msingi au haihitajiki kukusanya taarifa kutoka kwako tu au pale tunapolazimika au kuidhinishwa kufanya hivyo kisheria.

Pia, So They Can inakusanya taarifa kutoka upande wa tatu ambao wanatuchangia sisi au wanaratibu msaada mahali pa kazi. Kama mtu yeyote atachangia kwa niaba yako, na akaomba kwamba upewe taarifa kuhusu zawadi zao, tutachukua taarifa walizoziwasilisha kukuhusu.

NAMNA YA KUZITUMIA TAARIFA

Taarifa zako binafsi zitatumika na kutolewa kwa madhumuni ya kuzikusanya tu au vinginevyo kulingana na Sheria ya Usiri. So They Can inaweza kukusanya taarifa zako binafsi kwa madhumuni mbalimbali ikiwamo:

- Uchangishaji fedha:
    a) kushughulikia au kuthibitisha mchango wako na kutoa risiti;
    b) kutoa taarifa ya namna mchango wako ulivyotumika;
    c) kukufahamisha ikiwa tuna taarifa ambazo zinaweza kuathiri ufadhili wako;
    d) kushughulikia maswali, maoni, pongezi na malalamiko yako;
    e) kukufahamisha kuhusu fursa mpya za kufadhili shughuli zetu;
    f) kuchambua shughuli za mfadhili ili kumarisha ufanisi wetu.
- Kujitolea na misaada mingine: kukuwezesha kutusaidia katika kujitolea, kuchangisha fedha, kuongeza uelewa na shughuli nyingine zinazohitaji msaada.
- Kujitangaza: kuwasiliana na wewe kuhusu miradi, mafanikio na matokeo yetu, matukio yajayo na yaliyopita.
- Masuala mengine: kuwasiliana nawe kuhusiana na uendeshaji, shughuli na malengo yetu, kuthibitisha utambulisho wako, kuboresha na kutathmini programu na huduma zetu na kuendana na sheria zinazohusika.

Pale ambapo So They Can inakusanya taarifa zako binafsi kwa madhumuni maalumu ambayo hayajabainishwa hapo juu, tutakupatia notisi inayoeleza madhumuni ya msingi na madhumuni hayo mengine ambayo yanahitaji kukusanya taarifa zako binafsi.

NI WAKATI GANI TUNATOA TAARIFA

So They Can haitatoa taarifa zako isipokuwa kama moja wapo kati ya yafuatayo yatatokea:

- umeridhia kutoa taarifa (kwa taasisi ya tathmini ya mkopo, taasisi za uchunguzi, kwa ajili ya madhumuni mengine).
- zinatakiwa au zimeidhinishwa na vyombo vya serikali na mashirika ya utekelezaji wa sheria.

VIDAKUZI, TOVUTI NA SERA YETU YA USIRI

Ili kuelewa namna watu wanavyoingia na kutumia tovuti ya So They Can na majukwaa mengine ya mitandao ya kijamii yanayohusiana na tovuti yetu na namna wanavyoitumia tunategemea vidakuzi (cookies) vinavyotolewa kutoka upande wa tatu. Hii inatusaidia kupima ufanisi wa matangazo yetu ya mtandaoni. Vidakuzi havitoi taarifa zako binafsi kama jina lako, anwani, namba ya simu au baruapepe. Unaweza kubadilisha kivinjari chako ili kuzuia vidakuzi lakini kufanya hivi kunaweza kuzuia uwezo wako wa kuingia katika baadhi ya maeneo katika tovuti yetu.

NAMNA YA KULINDA TAARIFA

So They Can inachukua hatua za kuzilinda taarifa binafsi dhidi ya kutumiwa vibaya, kuharibiwa au kupotea; na kupatikana kwa wasioidhinishwa, kurekebishwa na kutolewa kwa watu wengine.

Tunatumia fomu za usalama za mrejesho ili kulinda taarifa za mhusika na za kifedha ulizotupatia kupitia mtandaoni. Ili kuhakikisha kwamba kivunjari chako kinaendana na mifumo yetu, hakiki alama ya usalama (mara nyingi ni alama ya kufuli) upande wa chini wa skrini yako.
Tunaulinda mfumo wetu wa TEHAMA kwa kutumia kidhibiti mtandao na skana za programu za kudhibiti virusi. Pia tunahakikisha kwamba taarifa binafsi zinaondolewa katika kompyuta kabla ya kuzitupa au kuziuza.
Mafaili ya nakala ngumu yanatunzwa katika makabati na wafanyakazi wanapewa mafunzo kuhusu taratibu zetu za usiri. Ni wafanyakazi walioidhinishwa pekee wanaoweza kuona taarifa zako na ni pale tu inapohitajika.

UNAWEZAJE KULINDA TAARIFA ZAKO

Kama unafadhili mtoto au mtu mzima kupitia ufadhili wa So They Can tafadhali hakikisha unafuata mwongozo wa So They Can kuhusu kuwasiliana na kumtembelea mtu anayefadhiliwa ili kuhakikisha usiri unadumishwa. Mawasiliano kati yako na mtu unayemfadhili yanapaswa kupitia ofisi ya So They Can iliyopo Australia au New Zealand. Hii inajumuisha lakini bila kikomo katika kutuma mawasiliano ya kielektroniki, mtandaoni na kutembelea ana kwa ana.

TUNATUNZA TAARIFA ZAKO KWA MUDA GANI

So They Can litaharibu au kuondoa utambulisho wa taarifa zako binafsi inapotokea hazihitajiki tena kwa madhumuni yaliyokusudiwa isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo na sheria.

KUPATA TAARIFA ZAKO BINAFSI

Una haki ya kupata taarifa zako zote binafsi ambazo zimekusanywa na kuhifadhiwa na So They Can. Kuomba kupata taarifa zako tafadhali wasiliana nasi kwa kutumia mawasiliano yaliyobainishwa hapa chini.

KUJITOA KATIKA MAWASILIANO

Kama hutaki kupokea mawasiliano au taarifa zetu za kujitangaza tafadhali wasiliana nasi kwa kutumia mawasiliano yaliyobainishwa hapa chini.

TAARIFA YA LAZIMA YA UVUJAJI WA DATA

Kwa mujibu wa Sheria ya Usiri ya nchini Australia So They Can kwa kushirikiana na Kamishina wa Taarifa wa Australia linatakiwa kukutaarifu ikiwa wanashuku kwamba data zimevuja (zinazohusu taarifa zako binafsi na/au taarifa nyeti) na kwamba kuna hatari ya kutokea madhara makubwa kwako kama matokeo ya uvujaji wa data.

MALALAMIKO

Kama una maswali yoyote au ungependa kuwasilisha malalamiko kuhusiana na Sera ya Usiri au namna tunavyotunza taarifa zako binafsi, tafadhali wasiliana nasi kupitia +61 2 9966 5225, tutumie baruapepe kupitia info@sotheycan.org au tuandikie kupitia So They Can S.L.P. 422 Crows Nest NSW 1585.

Tunawajibika kushughulikia malalamiko na maswali ndani ya siku kumi na nne tangu kupokelewa. Kama hujaridhishwa na majibu yetu, unaweza kuwasilisha malalamiko katika Ofisi ya Kamishina wa Taarifa Australia (OAIC) na kuandika kwa OAIC katika GPO S.L.P. 5218 Sydney NSW 2001. Kwa taarifa zaidi kuhusu OAIC, tafadhali fungua tovuti kwa anwani www.oaic.gov.au.

NYARAKA ZINAZOHUSIANA NA SERA HII

Sera na Mwongozo wa Rejista wa So They Can